JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

*Unapojibutafadhalitaja:*

**KUMB.NA. MCPF.1414/15** **22 Januari, 2026**

Wananchi wote,

Wilaya ya Ilemela,

**ILEMELA - MWANZA.**

Yah: **TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa mujibu wa Kanuni ya 110 – 113 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi ifuatatyo-:

**MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA – NAFASI MOJA (01)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe ni Raia wa Tanzania, Mkazi wa Kawaida wa Manispaa ya Ilemela,
ii. Awe muadilifu na muaminifu,
iii. Awe na Taaluma katika mojawapo ya fani zifuatazo
    - Menejimenti ya Rasilimali watu (Human Resources Management)
    - Utawala wa Umma (Public Administration)
    - Sheria (Law).
iv. Awe mstaafu Serikalini
v. Awe na umri kuanzia miaka 55 hadi 65.

**Majukumu ya Mwenyekitiwa Bodi ya Ajira:**

- Kuongoza Vikao vya Bodi ya Ajira kwa mujibu wa Taratibu za Vikao
- Kusaini mihitasari ya Kikao cha Bodi ya Aiira.

**STAHIKI**

- Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atalipwa stahiki za Kikao kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Serikali Na.2 wa mwaka 2010 wenye Kumb Na.C/AC.17/45/01/125 wa tarehe 11/02/2010 ukisomwa kwa pamoja na Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 4 wa Mwaka 2014 wenye Kumb Na CAC.1 7/45/01/G/103 wa tarehe 02/12/2014.

OfisiyaMkurugenziwaManispaa, HalmashauriyaManispaaIlemela, 200 Br. yaBuswelu, 33282 Buswelu, S.L.P 735 Ilemela ,Mwanza. Simu: + 255 (28) 2981196, Nukushi: + 255 (28) 2981196,
Baruapepe: md@ilemelamc.go.tzTovuti: www.ilemelamc.go.tz
*(BaruazotezitumwekwaMkurugenziwaManispaa)*

CB/JB

**Muda wa kutumikia nafasi.**

Kwa kuzingatia Kanuni ya 113 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atahudumu kuanzia tarehe ya kuteuliwa mpaka pale litakapovunjwa Baraza la Madiwani (***Kipindi kisichozidi miaka mitano)***

**Masharti ya jumla ya Mwombaji:**

- Awe Raia wa Tanzania.
- Waombaji waambatanishe vivuli vya vyeti vyao vya shule, Taaluma, kuzaliwa/ kitambulisho cha Uraia (NIDA) na Wasifu (Curriculurn Vitae).
- Kila Mwombaji aambatishe picha ndogo (Passport size) ya hivi karibuni
- Kila Mwombai aandike kwa usahihi, Anuani yake na namba ya simu inayopatikana muda wote.
- Mwombaji asiwe kiongozi wa Chama chochote cha siasa.
- Mwombaji awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la jinai.

**Maombi yote yatumwe kwa:**

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa.
S.L.P 735,
**ILEMELA.**

***Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 04/02/2026.***

Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela www.ilemelamc.go.tz

Imetolewa na:

Dr. Maria E.Kapinga

**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA**

**ILEMELA.**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA S.L.P 735 MWANZA.

**Nakala**: Mbao zote za matangazo za Manispaa.



CB/JB

CamScanner